

## Mdhihiriko wa Vionjo vya Fasihi ya Kisasa katika Nyimbo za Taarabu

Hassan, R. Hassan  
Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro  
hassrash87@gmail.com

### Ikisiri

Makala hii inahusu mdhihiriko wa vionjo vya fasihi ya kisasa katika nyimbo teule za Taarabu. Data za msingi zilizofanuliwa katika makala hii zimepatikana maktabani kwa kutumia njia ya uchanganuzi wa matini. Nadharia ya Usasa imetumika kama kiunzi muhimu katika ukusanyaji, uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika makala hii. Makala imebaini kuwa nyimbo za Kiswahili za Taarabu zina ukwasi wa vionjo ambavyo vinaziweka katika kapu la fasihi ya kisasa. Vionjo hivyo ni pamoja na mwanzo wenye kiitikio chenyesauti kali na zenye vishindo, matumizi ya mbinu ya cheba, matumizi ya maneno ya mtaani na matumizi ya nyenzo za kisayansi na kiteknolojia. Nyimbo hizi zimekuwa zikitumia mashairi ya mipasho, mwingiliano wa wimbo ndani ya wimbo, kuchanganya ndimi na kuhitimishwa na sehemu ya ngoma chini. Makala hii inahitimisha kwamba nyimbo za Kiswahili za Taarabu zimefumbata vionjo vya kisasa ambavyo vinazifanya kuwa na mabadiliko makubwa na kuzidi kujiimarisha kwa hadhira ya sasa.

**Maneno Msingi:** Vionjo, Nyimbo, Fasihi ya Kisasa na Nyimbo za Taarabu.

### Utangulizi

Kwa muda mrefu, tanzu mbalimbali za fasihi zimekuwa katika mwendo wa mabadiliko. Mabadiliko haya yanaenda sanjari na mageuzi yanayoikumba jamii katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kitamaduni na kifikra (Mulokozi, 2017). Suala hili linajidhihirisha zaidi katika tanzu za tamthiliya, ushairi na riwaya. Tanzu hizo zilingiza vionjo vipya ambavyo havikuzoeleka hapo awali. Katika muktadha huo, nyimbo kama utanzu mmojawapo wa fasihi simulizi umekuwa ukipokea vionjo vipya. Wataalamu mbalimbali waliotafiti kuhusu dhana ya vionjo vya fasihi ya kisasa wamejiegemeza katika tanzu za fasihi andishi. Baadhi yao ni Senkoro (2006), Khamis (2007) na Samwel (2015). Licha ya kuwapo kwa tafiti hizo, dhana ya vionjo vya fasihi ya kisasa katika tanzu za fasihi simulizi bado hazijachunguzwa kwa kina. Makala hii imechunguza vionjo vipya vya fasihi ya kisasa katika nyimbo za Kiswahili za Taarabu.

MAKALA HALISI

HISTORIA YA MAKALA

**Kupokelewa:** 03 Agosti 2021

**Kurekebisha:** 30 Sept. 2021

**Kukubaliwa:** 29 Oktoba 2021

**Kuchapishwa:** 08 Dis. 2021

ISSN: 2453 – 6016

Juzuu 7,

Toleo 2,

pp. 1 – 10.

**NUKUU:** Hassan, H. R. (2021). Mdhihiriko wa Vionjo vya Fasihi ya Kisasa katika Nyimbo za Taarabu. *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences*, 7(2), 1 – 10.

Fasihi ya kisasa ni aina ya fasihi ambayo imeingiza vionjo vya kisasa katika usimulizi na uandishi wa kazi zake. Upya ni hali ya kitu aghalabu kufahamika mara ya kwanza; isiyo ya zamani. Khamis (2007) anafafanua fasihi ya kisasa kwa kuzingatia vionjo vya fasihi ya kisasa. Upya unaopatikana katika fasihi umo katika usanii na maudhui yake. Kisanaa, kuna mabadiliko mengi ya kushangaza na kutatiza muundo na vitomeo vyake vya fani na umbuji katika mbinu inayojaribu kuasi kwa makusudi uhalisi mkongwe, uhalisi mkavu. Mbinu ya fantasia, umataifa, usayansi na mabaki ya uchawi, ushirikina na mazingaombwe na hatimaye mwingilianomatini. Mbinu hizi zinakubaliana na kwenda bega kwa bega kabisa na maudhui mapya.

Fasihi ya kisasa hujulikana kutokana na sifa zake ambazo zinasawiri maisha tunayoishi sasa. Ijapokuwa Khamis Khamisi kaipa jina la fasihi mpya, bado inasawiri vionjo vinavyobebwa na fasihi ya kisasa. Makala hii inamakinikia vionjo vya fasihi ya Kiswahili vya kisasa vivavyojitokeza katika nyimbo za Kiswahili za Taarabu. Nyimbo hizi kwa kiasi kikubwa zimechota vionjo anuai vya fasihi ya kisasa ambavyo havikuwapo katika Taarabu ya kale.

### **Mbinu za Utafiti**

Makala hii imejadili vionjo vya fasihi ya kisasa vinavyojitokeza katika nyimbo teule za Taarabu. Matokeo ya makala hii yametokana na utafiti uliofanyika katika mwegamo wa kitaamuli uliojikita katika usanifu wa kifani. Usanifu wa kifani unahusu tafiti zinazolenga kuchunguza jambo fulani kwa kina ili kutumia matokeo ya uchunguzi huo kama kiwakilishi cha kuonesha hali ilivyo katika sehemu au jamii nyingine kama hiyo (Ponera, 2019). Uchunguzi ulifanyika maktabani ambapo nyaraka mbalimbali kama vitabu, tasnifu zilisomwa pamoja na kusikiliza nyimbo teule za Taarabu na kupata maarifa yaliyomo katika makala hii. Data zilizokusanywa ziliwasilishwa na kuchambuliwa kwa njia ya maelezo. Sampuli ya nyimbo kumi na mbili za Taarabu ziliteuliwa kama msingi wa kuchunguza mdhahiriko wa vionjo vya fasihi ya kisasa. Nyimbo hizo ni pamoja na wimbo wa *Mama wa Afrika, Mavituz na Majamboz, Mbona Watakereka Sana, Akh! Po! Chaurongo Nuksi X, Hapa Kazi Ipo* na *Mimi wa Karne ya 21*. Zingine ni *Hafagiliwi Mtu Hapa, Ngangari Feki, Sakata Lako, Kindumbwendumbwe, Wema* na *Alokutwika*. Uteuzi wa nyimbo hizo umetokana na kubeba upya wa kivionjo vya fasihi ya kisasa ambavyo vimedhahirika katika makala hii.

### **Kiunzi cha Nadharia**

Mjadala wa makala hii umeongozwa na nadharia ya usasa. Nadharia ya usasa ni tetemeko katika sanaa ambalo lilishuka kubadilisha muundo wa muziki, uchoraji, fasihi na usanifu wa majengo kabla ya karne ya ishirini (Barry, 1995). Sehemu iliyoathiriwa zaidi na tetemeko hili ni mji wa Vienna katika miaka ya 1890-1910, lakini madhara yake yalijitokeza zaidi katika maeneo ya Ufaransa, Ujerumani, Italia na Uingereza. Waasisi wa nadharia ya usasa ni Ezra Pound, Hulme na Eliot (Wamitila, 2002). Makala imezingatia mihimili mitatu ya nadharia hii ambayo ni kuanzishwa kwa uvumbuzi wa ujarabati wa mawazo mapya yasiyokubalika kwa

urahisi, kuanzisha vionjo vipya na kuendeleza utamaduni wa fasihi pendwa na kutukuza usasa au utamaduni wa kiulimwengu pamoja na kuendeleza mtindo unaofuata mtiririko wa mawazo (Mushengyezi, 2003). Utumiaji wa nadharia ya usasa ulitusaidia kuvichunguza vionjo vya fasihi ya kisasa katika nyimbo teule za Taarabu. Mihimili ya nadharia hii imefanikisha kuviibua vionjo vya fasihi ya kisasa vinavyojichomoza katika nyimbo za Taarabu.

**Vionjo vya Fasihi ya Kisasa Vinavyodhihirika katika Nyimbo Teule za Taarabu**  
Sehemu hii inabainisha na kuchambua kwa kina vionjo vya fasihi ya kisasa vinavyodhihirika katika nyimbo teule za Taarabu ya Kiswahili. Vionjo hivi vimefafaniliwa katika sehemu inayofuata.

### **Mwanzo Wenye Kiitikio**

Usasa katika nyimbo za Taarabu za Kiswahili unadhihirika vizuri kupitia mwanzo wake. Jahadhmy (1966) anabainisha kuwa hapo zamani nyimbo za Taarabu zilikuwa ni za taratibu na polepole. Mwendo huu ulikuwa ni kuanzia mwanzo wa wimbo mpaka mwisho wake. Hali hii ni tofauti na nyimbo za sasa. Kwa mujibu wa nyimbo tulizozichunguza tunaona kuwa nyimbo nyingi zinakuwa na mwanzo wenye kiitikio chenye sauti kali na zenye vishindo. Khatib (2014) anaeleza kuwa mwanzo wa namna hii kwa kiasi kikubwa hukusudiwa kuvuta makini ya hadhira na kujiandaa kusikiliza mashairi yaliyomo ndani ya wimbo husika. Mabadiliko haya ya kimianzo yanatoa sura mpya ya nyimbo za Taarabu katika sikio la hadhira. Mathalani, wimbo wa “*Mavituz na Majamboz*” ulioimbwa na Haji Mohamed katika kundi la *The East African Melody* unasawiri vizuri usasa huo katika mwanzo wake:

Heee! Mavituz,  
Heee! Majamboz,  
Hey! Hey! Hey! Mavituz,  
Hey! Hey! Hey! Majamboz,  
Uchungu, uchungu, uchungu,  
Wanaona uchungu!

Mwanzo huo ambao unagonga masikioni mwa msikilizaji kutokana na sauti kali na yenye kishindo za waimbaji unasindikizwa na mapigo yenye nguvu ya ala za muziki na zinazokwenda kasi yaani kimchakamchaka (Mohamed, 2015). Mfano mwingine unaoshadidia hoja hii unatoka katika wimbo wa “*Mbona Watakereka Sana*” ulioimbwa na Zuhura Shaaban wa kundi la *The East African Melody*. Mwanzo wa wimbo huo ni huu:

Hamtuwashi,  
Hamtuzimi,  
Mwaona donge la nini,  
Kama mnaweza pandeni juu mkazibe,  
Wanadamu, walimwengu, kama yetu yawakera,  
Mbona watakereka sana,  
Na watakereka sana!

Katika mwanzo wa wimbo huo sauti ya waitikiaji inatolewa kwa ukali na kishindo kinachosindikizwa na ala za muziki. Mifano hiyo tulioidondoa inadhihirisha usasa katika nyimbo za Kiswahili za Taarabu. Usasa ambao unavuta makini na nadhari ya msikilizaji. Kionjo hiki kinamuandaa msikilizaji na kumfanya awe na hamu ya kutaka kujua mashairi ya wimbo mzima kutokana na mwanzo huu uliobeba sauti kali na yenye kishindo. Uanzishwaji wa mwanzo wa namna hii unaenda sanjari na nadharia ya usasa katika kuibua vitu vipya vinavyoendana na jamii ya sasa. Hivyo, hata nyimbo za Kiswahili za Taarabu kuanza kwa kishindo na sauti kali kunadhihirisha mwendo halisi wa jamii inayotumbuizwa.

### **Mbinu ya Cheba**

Khatib (2014) anafafanua cheba kuwa ni mbinu ya kisanaa inayotumika katika mianzo ya nyimbo za Taarabu ambapo huhusisha usemaji wa mwimbaji kisha hufuata uimbaji. Cheba ni tofauti na kughani. Mbinu hii ya cheba hukoleza usasa na mvuto mkubwa wa Taarabu. Mfano wa cheba tunauona katika wimbo wa “*Akh Po! Cha Urongo Nuksi X*” ulioimbwa na Mwanahawa Ali katika kundi la *The East African Stars*. Katika wimbo huu, mwimbaji anaanza kwa mbinu hii ya cheba kwa kusema:

Halo! Halo!  
Ammaaah! Shughuli imempata.

Baada ya cheba hiyo, sauti za waitikiaji hufuata kwa kiitikio chenye maneno yafuatayo:

Nuksi yule, hana dogo pale alipo,  
Bora angetafuta ajira, shirika la upelelezi.

Mbinu ya cheba pia inajitokeza katika wimbo wa “*Ngangari Feki*” ulioimbwa na Khadija Yusuf. Wimbo huu unaanza kwa cheba yenye kuhusisha kicheko cha waitikiaji na majibizano baina ya mwimbaji na waitikiaji kama ifuatavyo:

Waitikiaji: Hehehehe! Hata nawe ngangari?  
Mwimbaji: Nashangaaaaa!  
Waitikiaji: Ovyooooo kama mchuzi wa magozi.

Mifano hiyo inadhihirisha matumizi ya cheba kama mbinu mpya ya kuanza katika nyimbo za Kiswahili za Taarabu. Mbinu ya cheba kama asemavyo Khatib (2014) kuwa inakutanisha dhana ya mazungumzo hasa ya wanawake katika baraza zao. Suala hilo ni la kweli kwa sababu cheba imejengwa katika sura ya mazungumzo ya kawaida ambayo yanatumika ndani ya Taarabu. Baada ya cheba, hufuata kiitikio kirefu kabla ya mashairi ya wimbo wenyewekuanza kuimbwa. Mbinu hii ni ya kisasa kwani hapo awali hasa katika Taarabu asilia mbinu hii haikuwa ikitumika. Taarabu asilia ilikuwa ikitumia mbinu ya mianzo ya kughani ambapo mwimbaji huanza kwa kuwa katikati baina ya kuzungumza na kuimba (Mohamed, 2015). Aidha, zilitumia mwanzo wa moja kwa moja kwa mwimbaji kuanza kuimba mashairi ya wimbo husika. Vilevile, zipo Taarabu zilizoanza kwa kucharazwa kwa vinanda vya taratibu kabla ya mwimbaji kuanza kuimba.

### **Maneno ya Mtaani**

Mashairi ya Taarabu ya zamani yalikuwa yanatumia maneno teule na fasaha na mengi yakiwa yana asili ya Kiarabu (Khatib, 2014). Utumizi wa maneno hayo ulitokana na athari ya Kiarabu ambayo haikuepukika katika nyimbo za Taarabu (Jahadhmy, 1966). Hivi sasa Taarabu imechukua mkondo mpya kwa kuchopeka kionjo cha maneno ya mtaani katika mishororo ya beti zake. Maneno ya mtaani ni maneno yasiyo rasmi ambayo hutumiwa aghalabu na vijana wa mtaani (Mwansoko, 1981). Nyimbo za Taarabu za kisasa zimekuwa na matumizi makubwa ya maneno ya mtaani katika utunzi wake. Matumizi haya ya maneno ya mtaani hukusudiwa kutoa mvuto kwa hadhira ya wakati huu. Tukiurejelea wimbo teule wa “*Ngangari Feki*” tunaona ukidhihirisha kionjo hiki katika baadhi ya mishororo ya ubeti wa utangulizi. Katika ubeti huo, sauti za waitikiaji zinaimba mishororo ifuatayo:

Wataka kuleta soo wewe, nimekushtukia wewe,  
Wataka nipiga bao wewe, uninyang’anye mwandani wewe,  
Ili awe mchumba wako, ili awe mchumba wako,  
Ni ndoto za alinacha, kwa hapa utabloo.

Aidha mekubaini, juzi usiku wa mwezi,  
Megonga madirishani, nimo ndani na mpenzi,  
Ukapiga chabo ndani, nakuchora mpuuzi,  
Katu huyu humchuni, si buzi la pata sote.

Kupitia beti hizo tunaona maneno ya mtaani yakitumika kama soo (jambo lenye madhara/janga), utabloo (utashindwa), kupiga chabo (kuchungulia), nakuchora (nakutazama), humchuni (humlii fedha zake) na buzi (mwanamme anayehonga). Aidha, wimbo wa “*Hapa Kazi Ipo*” ulioimbwa na Mariam Khamis akiwa na kundi la Zanzibar Stars nao umetumia kwa kiasi kikubwa maneno ya mtaani. Mfano ubeti ufuatao:

Magumashi acha longolongo, hapa kazi ipo tu,  
Usipime kabisa, huyu mtu wangu,  
Hii bahati yangu nimeopoa dume la mbegu,  
Mambo bomba funika, funika bovu.

Katika ubeti huo tunaona maneno kama magumashi (mambo ya udanganyifu), longolongo (vitu visivyo na uhakika), usipime mtu wangu (usijaribu), mambo bomba (mambo mazuri) na funika bovu (kutia fora) yakitumika. Haya ni maneno yaliyotamalaki mno katika mazungumzo ya vijana wa mtaani. Kutumika kwa maneno hayo ndani ya nyimbo za Taarabu kunaichota hadhira ya vijana na kufanya nyimbo hizo zipendwe na watu vijana wa jinsia zote. Pia, kionjo hiki kinaikurubisha Taarabu na jamii kwa sababu maneno ya mtaani yanatokana na jamii.

### **Nyenzo za Kisayansi na Kiteknolojia**

Mrikaria (2012) anaeleza kuwa mchakato wa kuiendesha dunia kupitia sayansi na teknolojia umeleta mabadiliko na mwingiliano katika fasihi simulizi ya Kiswahili. Mabadiliko haya yanasawiriwa vizuri katika nyimbo za Taarabu. Watunzi wa mashairi ya nyimbo za Taarabu za Kiswahili wa zama hizi katika utunzi wao wanaonesha kwenda sanjari na maendeleo ya sayansi na teknolojia kivionjo. Vionjo

vya kisayansi na kiteknolojia vimesababishwa na utandawazi. Kiutamaduni, utandawazi unahusishwa na kuenea kwa tamaduni za Kimagharibi kwa njia ya maingiliano, hususani ya kibiashara au mtiririko wa muziki na taswira kupitia video, televisheni, mitandao ya kompyuta, simu, CD, DVD na VCD (Khamis, 2007). Nyimbo za Taarabu ya kisasa kama sehemu ya fasihi nazo hazipo nyuma katika kusawiri kionjo hiki cha matumizi ya nyenzo mbalimbali za kiteknolojia. Hii inatokana na ukweli kuwa kwa watunzi wa sasa ni vigumu kukwepa kutumia kionjo hiki kwa sababu wanatunga kazi zao katika karne ya maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kompyuta kama nyenzo ya kiteknolojia inabainika katika beti za nyimbo mbalimbali za Taarabu. Mfano, katika mashairi ya wimbo wa “*Mimi wa Karne ya 21*” ulioimbwa na Khadija Yusuf tunaona jinsi programu za kompyuta zikitajwa. Mwimbaji anasema:

Nitazameni wa karne nimeingia,  
Mimi ni top ten nimeingia,  
Nafanya maintenance, kwa software,  
Nafanya maintenance, kwa hardware,  
Microsoft style naichezea.

Katika mishororo hiyo tunaona jinsi programu za kompyuta zikitajwa waziwazi. Hii inadhihirisha wazi kuwa nyenzo ya kompyuta kwa watunzi wa nyimbo za Taarabu inafahamika. Wimbo wa “*Hafagiliwi Mtu*” ulioimbwa na Zuhura Shaaban nao unataja nyenzo ya kompyuta na utendakazi wake katika mawasiliano kama vile kutuma baruapepe. Mwimbaji anatoa:

Wajifanya master plan, mkuu wa teknolojia,  
Una mbinu kalikali, bibi kujifagilia,  
Unatumia email, kuwasiliana na dear,  
Sometimes mobitel, pia unampigia.

Katika ubeti huo tunaona huduma ya baruapepe ambayo iliasisiwa na kifaa cha kompyuta ikitajwa kama mbinu ya teknolojia. Kwa upande wa televisheni kama nyenzomojawapo ya sayansi na teknolojia haikuachwa katika nyimbo za sasa za Taarabu. Watunzi wamekisawiri kifaa hiki katika mashairi ya nyimbo zao. Kwa mfano, katika wimbo wa “*Sakata Lako*” ulioimbwa na Mwanahawa Ali unaeleza jinsi kashfa za mtu zilivyotangazwa katika magazeti mpaka kwenye televisheni. Mwimbaji anaimba:

Mtaani unasemwa kisonoko,  
Magazetini imeandikwa aibu yako,  
Redioni kumetangazwa kashfa yako,  
Televisheni imeonesha sakata lako.

Kupitia ubeti huo tunaona dhima ya televisheni kama chombo kimojawapo cha habari kikitoa taarifa za mlengwa kwa jamii. Televisheni pia tunaisikia ikitajwa katika wimbo wa “*Akh! Po! Chaurongo Nuksi X*” ulioimbwa na Mwanahawa Ali. Katika wimbo huu tunamsikia mtu mwongo na mbea akiambiwa waziwazi kuwa bora

angetafuta ajira katika vituo vya televisheni ili awe anaripoti habari. Mwimbaji anasema:

Bora angetafuta ajira, shirika la upelelezi,  
La Kimarekani, la FBI au CIA,  
Au ukawa ripota, wa televisheni,  
TBC, ITV, TVZ, redio za FM,  
Mungu atunusuru na shari za cha urongo,  
Karahi zake katika mtandao wa intaneti,  
Cha urongo nuksi, Loh! Loh! Loh! Kazi kwake.

Mifano hiyo inaonesha wazi mabadiliko ya kiteknolojia na sayansi yanayoikumba jamii yalivyopokelewa katika mashairi ya nyimbo za Kiswahili za Taarabu. Kuwapo kwa vifaa vya teknolojia kama vile kompyuta na mitandao kumeweza kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa urahisi (Mrikaria, 2002). Wanajamii nao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakizitumia nyenzo hizo katika maisha yao ya kila siku. Nyimbo za Kiswahili za Taarabu kubeba kionjo hiki cha kisasa kunafungamana na mawazo ya wanausasa katika kuunda zana za kisasa na kuziendeleza katika fasihi.

### **Kuchanganya Ndimi**

Hiki ni kionjo kingine cha kisasa kinachopatikana katika nyimbo za Kiswahili za Taarabu. Kuchanganya ndimi ni kuweka maneno yasiyo ya Kiswahili katika sentensi ya Kiswahili (Hamisi, 2021). Katika muktadha wa utunzi wa nyimbo za Taarabu za kisasa tunaona kuwa zikitumia maneno yasiyokuwa ya Kiswahili katika mishororo yake. Maneno hayo aghalabu huweza kuwa ya Kiingereza au ya lugha za kikabila. Katika wimbo wa “*Ngangari Feki*” mwimbaji anasema:

Huna power, power ya kunifikia,  
Huna nyenzo, nyenzo za kunipindua,  
Huna mpya, hasidi usojijua,  
Huna mpya, bwawa la kuogelea,  
Usiruke anga zangu, mimi nitakuzodoa,  
Mimi nitakuzodoa, ujutie kuzaliwa,  
Ewe ngangari feki take care.

Katika ubeti huo tunaona neno “*power*” likitumika kwa maana ya “nguvu” na “*takecare*” kwa maana ya kuwa na tahadhari. Wimbo wa “Alokutwika” ulioimbwa na Mwanahawa Ali nao unachanganya ndimi kwa kutumia maneno ya Kiingereza katika mishororo yake. Katika ubeti wa kwanza mwimbaji anasema:

Reception yako mbovu, havutiki nikwambie,  
Mimi nina perfect love, acha anizimikie,  
Endelea kuporoja, alokutwika bibi.

Maneno “*reception*” (mapokezi) yametumika kuashiria “sura/uso” na *perfect love*” kwa maana ya “penzi lililokamilika”. Uchanganyaji huu wa ndimi una dhima muhimu katika mashairi ya nyimbo hizi ikiwa ni pamoja na kusisitiza maudhui yatolewayo na kuupa upekee wimbo husika.

### **Sehemu ya Ngoma Chini**

Ngoma chini ni sehemu ya mwisho ya wimbo wa Taarabu. Sehemu hii aghalabu huwa inahusisha mabadiliko ya mapigo ya ala za muziki na kuwa katika hali ya kuchanganya na kuchangamka. Sehemu hii uhusisha ubeti ambao huimbwa na waitikiaji wote. Sehemu hii hupendwa sana na hadhira ya nyimbo hizi kwa kule kuchangamka kwake. Hadhira hucheza kwa kufuata mapigo ya sehemu hii pamoja na mashairi yaimbwayo (Mohamed, 2015). Pia, maneno yatolewayo katika ubeti wa sehemu hii huwa na mvuto ikizingatiwa kuwa ndio sehemu ya mwisho kabla ya wimbo kumalizika. Nyimbo nyingi za Taarabu za kisasa zimechukua kionjo hiki muhimu na kuwa sehemu ya muundo wa nyimbo zao. Mathalani, wimbo wa “*Ngangari Feki*” sehemu ya ngoma chini inahusisha maneno yafuatayo:

Ngangari ngangari ngangari gani, ngangari gani, ngangari feki,  
Acha acha mtima nyongo, ngangari gani ngangari feki,  
Usicheze na mali yangu, ngangari gani ngangari feki,  
Cheza cheza na mwenye mali, ngangari gani ngangari feki,  
Utakufa nacho kijiba cha roho,  
Utamuona hivihivi, shaksiya laazizi,  
Mimi ninaye natamba naye, ngangari gani ngangari feki,  
Mimi ninaye napeta naye, ngangari gani ngangari feki,  
Ndo huyu hapa natanua naye, ngangari gani ngangari feki,  
Iliyobaki wewe uliye tu, ngangari gani ngangari feki.

Kifungio hicho cha ubeti wa ngoma chini katika wimbo wa “*Ngangari Feki*” ni kiashiria cha upya katika Taarabu ya sasa. Kipande hiki cha ngoma chini katika wimbo wa Taarabu licha ya kuchangamsha hadhira pia kinanogeshwa wimbo husika kutokana na mapigo yake pamoja na mashairi yanayosindikiza. Aidha, huwa ni kiashirio kuwa wimbo husika unaelekea tamati.

### **Hitimisho**

Kwa jumla, makala hii imejadili juu ya mdhihiriko wa vionjo vya fasihi ya kisasa katika nyimbo teule za Taarabu. Nyimbo za Kiswahili za Taarabu zimeonekana kupokea mabadiliko makubwa ya kivionjo katika utunzi wa mashairi yake. Mabadiliko hayo yanadhihirisha wazi kuwa fasihi si sanaa tuli kama maji kwenye mtungi bali ni sanaa iliyo katika mwendo. Mwendo ambao unachukuana kama ngozi na mwili na jamii husika. Kupitia mjadala uliofanywa ndani ya makala hii tumebaini kuwa nyimbo za Kiswahili za Taarabu zina ukwasi mkubwa wa vionjo ambavyo vinazifanya nyimbo hizi kuzidi kujiimarishia mapenzi yake kwa hadhira yake.

### **Marejeleo**

Abdalla, B. A. (2012). Athari za Mabadiliko katika Nyimbo za Taarabu: Lugha na Uwasilishaji. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Alawy, Z. M. (2007). Nyimbo za Mipasho za Taarabu Zinavyochangia Kudumisha Maadili ya Wazanzibari. Tasnifu Ndogo ya B. A (Ed), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.



- Barry, P. (1995). *Beggining Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. United Kingdom: University Press.
- Baudrillard, J. (1983). *Simulations*. New York: Columbia University.
- Farhan, I. (1992). *The History of Taarabu Music in Zanzibar*. Zanzibar: SUZA.
- Jumanne, A. (2016). Mabadiliko ya Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganisho wa Riwaya za Shaaban Robert na Said A Mohamed. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Hamisi, T. A. (2021). Matumizi ya Kuchanganya Msimbo na Ndimi katika Tamthiliya ya *Tanzia Partice Lumumba*. Tasnifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro.
- Hassan, H. R. (2019). Uumbufu wa Mwanamke katika Nyimbo za Kiswahili za Taarabu: Vipengele, Sababu na Athari Zake kwa Jamii. *Koja la Taaluma za Insia: Kwa Heshima ya Profesa Joshua S. Madumulla*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Ltd.
- Jahadhmy, A. A. (1966). *Waimbaji wa Juzi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Khamis, S. A. M (2007). Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha* Na. 5. Dar es Salaam: TUKI.
- Khamis, S. A. M. (2007b). Utandawazi au Utandawizi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai. *Kiswahili* Na.70:47-66. Dar es Salaam: TUKI.
- Khatib, M. S. (2014). *Taarabu Zanzibar*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- King'ei, K. G. (1996). Nafasi ya Nyimbo za Kiswahili za Taarabu katika Jamii ya Kisasa. *Kioo cha Lugha* Na. 2. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mohammed, O. S. (2015). Mabadiliko ya Uchezaji Yaliyoletwa na Taarabu ya Sasa. *Mulika* Na. 34. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.
- Mushengyezi, A. (2003). *Twentieth Century Literary Theory*. Kampala: Mukano Bookshop Printing & Publishing Company Ltd.
- Mrikaria, S. E. (2012). Majukumu na Athari za Nyimbo za Watoto katika Enzi za Teknolojia ya Kidijiti: Mifano Kutoka Nyimbo za Watoto Nchini Tanzania. *Mulika* Na. 31. Dar es Salaam: TATAKI.
- Mwansoko, H. J. M. (1981). Aina za Mitindo katika Kiswahili. *Makala za Semina za TUKI*. Dare es Salaam: TUKI.
- Mzee, A. F. (2011). Athari za Nyimbo za Taarabu ya Mipasho kwa Jamii ya Wazanzibari. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

- Salum, S. (2007). Nyimbo za Taarabu Zinavyotoa Elimu na Mafunzo kwa Jamii ya Zanzibar. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).
- Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MEVELI Publishers.
- Senkoro, F. E. M. K. (2006). Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano Baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. *Kioo cha Lugha*, Na, 4: 22-38. Dar es Salaam: TUKI.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Focus Publication Ltd.
- Yego, E. K. (2013). Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarabu za Zanzibar. Tansifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.